CELEBRATING HOLINESS

CHURCH OF THE NAZARENE-AFRICA REGION

KISWAHILI

Januari 06, 2012

Mchungaji Mpendwa,

Neema na amani na iwe nawe kutoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana wetu Yesu Kristo!

Ningependa kutoa shukrani yangu kwa kuhusika kwako katika misheni ya kuwafanya Wanafunzi kuwa mfano wa Kristo katika Afrika. Kujitoa kwako katika kuhubiri Neno, kuomba na kuwaandaa watakatifu kwa ajili ya kazi ya huduma, kulinda washiriki na jukumu zingine zote zinazohusika na utawala na huduma ambazo unaendeleza juma baada ya juma zinatukuzwa mno. Asante kwa yote mnayofanya.

Kanisa la Mnazareti katika Eneo la Afrika linaendelea kupanuka na kukua. Tulisherehekea kufika kiwango cha idadi ya watu nusu milioni mwaka jana na kazi yetu katika nchi 42 juu ya nchi 54 za bara la Afrika. Hakika Mungu ametubariki kwa vile tumejitoa kwa kujenga kanisa Afrika!

Tunaposherehekea kupanuka na kukua kwa kanisa, ni muhimu kwamba tujikumbushe lengo letu la kimsingi kama dhehebu, ambalo ni kuhifadhi na kueneza utakatifu wa Kikristo kama vile ilivyoandikwa katika Maandiko, kupitia kwa kubadilishwa kwa wenye dhambi,

Kwa kutazama mbele, Kundi la Misheni la Jimbo la Afrika na Baraza la Halmashauri la Jimbo lilikutana mwezi wa Septemba 2011 ili kufikiria uamuzi ambao utahimiza kuendelea kwa uanafunzi mtakatifu, uinjilisti mtakatifu, utengenezaji wa uongozi, na maendeleo ya kanisa. Walipendekeza na kuithinisha uamuzi, “KUSHEREHEKEA UTAKATIFU”, wa mwaka wa 2012. Uamuzi huu haubadili mpango wako wa mwaka wa 2012, lakini ni wa kusifu na kuongezea kazi ya wakati huu ya kanisa la mtaa katika kuziidisha kuundwa kwa mazingira ya kiroho kwenye Jimbo la Afrika ambao Mungu amepewa uhuru wa kuleta uamsho wa utakatifu unaoendelea kwa makanisa yetu, kufanywa upya kwa kiroho kwa viongozi wetu na washirika. Tumetambua na kutengeneza raslimali za uamuzi huu ambazo tunatumai kwamba zitakuwa za msaada mkubwa kwako na kwa washirika wako.

Uamuzi huu utaanza siku ya Jumatano ya majivu, tarehe 22 Februari 2012, na wakati wa maombi ya kuazimia, kufunga, kusoma na uongozi wa kumbukumbu za Jumapili ya Pasaka tarehe 8 Aprili 2012. Kutoka siku ya Pasaka hadi Pentekoste, 8 Aprili – 27 Mei 2012, kanisa litaendelea na wakati wa kusoma na uongozi wa kumbukumbu kwa Utakatifu wa binafsi na wa ushirika kama vile inavyohusiana na tamaduni ya Uwesley na matokeo ya kutamani kila mhusika kuingia na kufanya upya uhusiano wa kimaagano na wa kuwajibika na Mungu na Kanisa

Lengo muhimu la uamuzi huu ni kwamba utakuwa ajenti ya kuchochea kanisa “kutafuta shirika takatifu la Kikristo kuokolewa kwa wenye dhambi utakatifu mkamilifu wa waumini, kujengwa kwao katika utakatifu, na kutafuta urahisi na kudhihirishwa katika Kanisa la kale la Agano Jipya. (*Kitabu cha Mwongozo Manual 2009-2013, Aya ya 25*)

P. O. Box 44, Florida 1710, South Africa ● Tel: +27-11-472-3615 ● Fax:+27-11-672-7614 ●E-Mail: nazarene@africa-region.org.za

Mchungaji, ningependa kukualika wewe pamoja na kanisa lako la mtaa kuhusika katika uamuzi wa Kusherehekea Utakatifu. Tafadhali somo orodha ya raslimali ambayo imejumlishwa katika pakiti hii au itapeanwa baadaye, na ujisikie huru kuwasiliana na Msimamizi wako wa Uwanda au ofisi yangu kwa msaada zaidi au ufafanuzi.

Asante kwa kuhusika katika Kusherehekea Utakatifu!

Dkt Filimao Chambo
Mkurugenzi wa Jimbo la Afrika
Kanisa la Mnazareti

P. O. Box 44, Florida 1710, South Africa ● Tel: +27-11-472-3615 ● Fax:+27-11-672-7614 ●E-Mail: nazarene@africa-region.org.za

Bara La Afrika

- Kunao nchi 54 katika bara la Afrika:
  - Nchi 48 za bara na mataifa 6 ya visiwa.

- Bara ya Afrika ndiyo bara la pili kwa ukubwa na pia la pili katika idadi ya watu:
  - Ukubwa wa bara la Afrika ni maili millioni 11.7 kwa mraba.
  - Idadi ya watu billion 1 (kulingana na takwimu za mwaka 2009)

Kazi ya Kanisa la Mnazareti – Takwimu:

- Kati ya nchi 54 za bara la Afrika, kanisa la Mnazareti linapatikana katika nchi 42.

- Kanisa lilianzishwa kaskazini mwa Afrika katika mji wa Cape Verde mwaka wa 1901

- Kanisa lilianzishwa kusini mwa Afrika katik nchi wa Swaziland mwaka wa 1910.

- Tangu mwaka wa 1901 na 1950 kanisa lilikuwa katika nchi nne pekee.

- Tangu mwaka wa 1950 hadi 1980:
  - Idadi ya ushirika ilikuwa = 37,000
  - Jumla ya nchi ambamo kanisa lilikuwa limeanzishwa = 9

- Tangu mwaka wa 1980 hadi 1990:
  - Idadi ya ushirika ilikuwa = 71,121
  - Jumla ya nchi ambamo kanisa lilikuwa limeanzishwa = 19

- Tangu mwaka wa 1990 had 2000
  - Idadi ya ushirika = 173,690
  - Jumla ya nchi ambamo kanisa lilikuwa limeanzishwa = 35

- Tangu mwaka wa 2000 had 2010
  - Idadi ya ushirika – 511,000
  - Jumla ya nchi ambamo kanisa lilikuwa limeanzishwa = 42

- Kazi ya Kanisa La Mnazareti ni mpya Afrika:
  - Asilimia 78.5 ya kazi ilifanywa pengine miaka 30 iliyopita ama miaka michache kuliko 30.
  - Asilimia 61 ya kazi ilifanywa miaka 20 iliyopita, ama miaka michache kuliko 20

- Leo kunao wilaya 125 ambazo zimegawanyika katika maeneo saba, maeneo saba, maeneo haya ni kama yafuatayo:
  - Eneo la Kati
  - Eneo la Mashariki
  - Eneo la Pembe la Afrika
  - Eneo la Ufaransa
  - Eneo la Katikati
  - Eneo la Kusini
  - Eneo la Magharibi

- Kunao:
  - Makanisa 4,237yaliyostawi na 4,195 ambayo hayajastawi.
  - Takribani viongozi 4000 wa dini wamehitumu barani kote.
  - Wakufunzi zaidi ya 6,750 wamo katika mashirika ya Mnazareti wakijitayarisha kuhitumu kuwa wachungaji.
  - Zaidi ya Washirika 549 000

CELEBRATING HOLINESS

CHURCH OF THE NAZARENE-AFRICA REGION

MWAKA WA 2012

MAOMBI NA KUFUNGA
TAREHE: MAJUMA SITA
FEBRUARI 22 – APRILI 08

KUSHEREHEKEA UTAKATIFU
TAREHE: MAJUMA SABA
APRILI 08–MEI 27 2012

VYOMBO VYA MAOMBI

- **Namna ya Kuomba**
- **Kalenda ya Maombi**
- **Maombi ya Kutembea**
- **Kilele cha Maombi**
- **Onyesho la Maombi na Sifa**
- **Saa Inayobadilisha Ulimwengu**

VIDEO Kutoka Kwa Dkt Chambo

Vifaa Vya Familia Yote

***Majuma Saba Ya Masomo Biblia* kwa maisha mwanzo ya utoto, ya msingi, ya ujana na utu uzima**

Mwongozo Wa Kufunga
Muhtasari Wa Mahubiri
Jinsi Ya Kuanza Mwongozo Wa Kundi Ndogo

Raslimali Zilizochapishwa Katika lugha ya

- ***Amharic***
- ***Chichewa***
- ***Kiingereza***
- ***Kifaransa***
- ***Kimalagasi,***
- ***Kireno***
- ***Shangaan***
- ***SiSwati***
- ***Swahili***
- ***Kihispania***

KWENYE MTANDAO
www.africanazarene.org